

SALA NA AHADI

YA WA WANAFUNZI WALIOSOMA DON BOSCO

Mungu Baba Mwenyezi kwa njia ya Mwanao Bwana wetu Yesu Kristu, na maombezi ya Mtakatifu Yohane Bosco usikilize sala za vijana waliopitia malezi ya Don Bosco popote ulimwenguni;

Tunakushukuru kwa tunu isiyofutika ya elimu ambayo tumeipokea chini ya malezi ya

Wasalesiani na kuwa chachu katika maisha yetu.

TUNAKUOMBA KWA UAMINIFU WA KIFAMILIA

- Utupe nguvu na ujasiri kuuishi ujumbe wa **utu** na wa **kisalesiani** kila siku katika jamii tunayoishi,
- Utusaidie tuwe Wachamungu na Raia waaminifu,
- Tusaidie kuishi pamoja na kukuza mshikamano ndani na nje ya Umoja wetu,
- Utuimarishe katika Imani, Matumaini na Mapendo.

TUNAAHIDI

- Kupigana na dhurma, usaliti, unafiki,uzembe na tabia ya kutokujali,
- kutetea kwa gharama yoyote ile, maadili yaliyotokana na mafundisho ya Don Bosco, hasa uhuru na ukweli kwa moyo wa kujitolea kijamii, kisiasa na kiuchumi,
- na kuwa, “chumvi ya dunia na nuru ya ulimwengu” yenye ushawishi mkubwa duniani na katika utume wa Wasalesiani.

TUNAOMBA

Uilinde familia ya Wasalesiani, Wapendwa wetu na kila mmoja wetu. **Amina**